**TAARIFA YA ZIARA YA WATAALAM NA WADAU WA MAENDELEO YA KUTEMBELEA MAENEO YA KIMKAKATI KWA AJILI YA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI TAREHE 11/01/2018**

**UTANGULIZI**

Mnamo tarehe 11/01/2018 wageni kutoka Unit Trust of Tanzania (UTT) walifika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kwa kufuatilia mazungumzo yao ya awali na Mkurugenzi Mtendaji , Lengo lao kuu ikiwa ni kuona maeneo ambayo yanaweza kufaa kwa uwekezaji na kuhakiki mambo kadhaa waliyozungumza na Mkurugenzi ili kupata ushiriki katika kuiwezesha Halmashauri kuwekeza na ama wao kuwekeza katika Halmashauri.

Aidha, wakati wa ugeni huo Afisa Mipango Bw. Muheranyi na Afisa Aridhi Bw. Cosmas waliitwa na kushiriki mazungumzo mafupi yaliyofanyika Ofisini kwa Mkurugenzi na kisha wageni na maafisa hao walianza safari ya kuelekea maeneo lengwa.

Maeneo yaliyotembelewa ni eneo la Benaco la maegesho ya magari ‘Parking Bay’, eneo la Lumasi (Industerial Park) lililoko Rwakalemera eneo lililokuwa na wakimbizi, Ngara garden na Eneo la Arab Global Nakataunga.

**WAJUMBE WALIOTEMBELEA MAENEO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ndg. Sypriani G. Muheranyi | - | Mtaalam wa Mipango | - H/W Ngara |
| Ndg. Cosmas Mchunguzi | - | Mtaalamu wa Aardhi | - H/W Ngara |
| Ndg. Shakiru Abdulkarim | - | Afisa kutoka UTT | - SLP 77783 Dar. |
| Bi. Eugenia Simon | - | Mkurugenzi Mkuu UTT | - SLP 77783 Dar. |

**MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA NINI LA KUFANYA KWA KILA ENEO LILILOTEMBELEWA**

**Eneo la Benaco kwa ajili ya maegesho ya magari ‘Parking Bay’**.

Timu hii baada ya kutembelea eneo hili wataalam wa UTT walishauri kuwa eneo hili liwekwe kwenye mchoro na kuonesha ni vitu gani vitakuwa ndani ya eneo la maegesho ‘Arctectural plan’ na gharama za kila kilichopo kwenye mpango mfano; Hotel ya kuhudumia wenye magari, maegesho ya magari, maeneo ya kuegesha aina ya magari, maeneo ya kutolea huduma ya chakula, maosheo ya magari, maeneo ya kufanyia services za magari ikiwa ni pamoja na kuongezea upepo n.k. Aidha, walishauri kwa huduma ya chakula Halmashauri ijenge vibanda na ku out source kwa watoa huduma.

Baada ya hapo watatumiwa nyaraka hizo kisha wataamua ama kuwekeza wenyewe na ama kutuunganisha na wawekezaji wanaowafahamu wao, baada ya kupitia na kuona ni kipi kinaweza kuanza na kipi kinaweza kuja baadae na gharama zake. Aidha, walisema kutuma kwetu nyaraka hizo mapema kutafanya nao kuchukua hatua mapema.

**Eneo la Lumasi 'Lukole' kulikokuwapo wakimbizi**
Hili lilionekana kuwa na baadhi ya miundo mbinu kama barabara na ni kubwa la kufaa kwa viwanda na baadhi ya sehemu za eneo hili kuwa za makazi ya watu, wakiwemo wamiliki na watumishi viwandani.

Ushauri ulitolewa kuwa hatua za Halmashauri kumiliki kihalali eneo hili zifanyike ikiwa ni pamoja na kupima eneo hilo na kuwekwa wazi ukubwa wake kwa uhalisia na mipaka.

**Eneo la 'Ngara Garden**
Kwa ajili ya eneo hili kuwa mjini lilivutia wataalam wa UTT kwamba kunaweza kuwekwa kitega uchumi ambacho Halmashauri ikiwekeana Mkataba na Mwekezaji akajenga na baadae kulipa ushuru 'mapato' kwa Halmashauri kwa kipindi Fulani na baada ya kipindi hicho inakuwa mali ya Halmashauri. Japokuwa kwa wakati huu hawakuwa na la zaidi kwa maeneo ya Garden.

**Eneo la Arab Grobal 'Nakatunga'**
Kwa upande wa eneo hili baada ya kulikagua kwa makini ulitolewa ushauri kuwa kunapaswa kuwekezwa aidha kwa kushirikisha shirika la Nyumba na makazi ili kupata namna nzuri ya kupata majengo yenye hadhi na thamani stahili.